SHULE YA SEKONDARI SEUTA
S.L.P. 30
SONGE – KILINDI
SIMU: 0783655357

Kumb. Na. SSS/JI/VO.II/2020 14/12/2020

JINA LA MWANAFUNZI.....
SHULE YA MSINGI ALIKOTOKA.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SEUTA KUANZA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

1.0. UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na Kidato cha kwanza katika shule hii ya Sekondari Seuta mwaka 2021. Shule ya Sekondari Seuta ipo Wilaya ya Kilindi Mkoa wa Tanga. Ipo umbali wa Km. 1 kusini mwa Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi.

Unatakiwa kuripoti hapa shuleni siku ya tarehe 11/01/2021 saa moja kamili asubuhi. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 15/01/2021. Utakapokuwa shuleni utakuwa na wajibu wa kusoma kwa bidii, kutii sheria za shule vilevile kushiriki shughuli zote za ndani na nje ya darasa kulingana na ratiba ya shule.

2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZI NGATIA

2.1. SARE ZA SHULE KWA WAVULANA

i. Suruari mbili za rangi ya kijani mpauko zenye marinda mawili kila upande, mfuko mmoja wa nyuma. Suruali zisiwe za kubana (sampo ya kitambaa imeambatanishwa).
Tahadhari: Hatutapokea mwanafunzi aliyeshona suruali kihuni mfano. Vimodo au suruali bila marinda.

ii. Shati jeupe lenye mikono mifupi
Tahadhari: Hatutapokea mwanafunzi mwenye shati la kubana, rangi iliyokolezwa na madawa, au shati fupi ambalo mwanafunzi atashindwa kulichomekea.

iii. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufungwa na kamba, visiwe na visigino virefu.

iv. Sweta, rangi ya bluu.

v. Soksi nyeusi jozi mbili.

2.2. SARE ZA SHULE KWA WASICHANA

i. Sketi mbili rangi ya zambarau zenye marinda mengi yanayozunguka sketi yote, kitambaa kiwe kizito (sampo ya kitambaa imeambatanishwa).

ii. Blauzi mbili nyeupe zenye mikono mifupi.

iii. Viatu vyesi vya ngozi vya kufungwa na kamba, visiwe na visigino virefu.

iv. Stocking (soksi ndefu) nyeupe jozi mbili.

v. Sweta rangi ya bluu.

vi. Kwa watakao vaa hijabu rangi ya kitambaa cha hijabu ifanane na rangi ya sare ya shule (blauzi)

2.3. MICHEZO

WAVULANA

i. Flana moja ya bluu
ii. Bukta ya rangi ya bluu.
iii. Raba

WASICHANA

i. Flana ya bluu
ii. Raba

2.4. VIFAA VYA DARASANI

i. Madaftari kumi na tano (15) makubwa
ii. Mkebe wa vifaa vya hisabati (mathematical set).
iii. Kalamu ya risasi (penseli) moja
iv. Rula moja
v. Kalamu

3.0. Pamoja na barua hii naambatanisha

i. Sheria za shule.

ii. Fomu ya mwanafunzi kupima afya kabla ya kujiunga na shule. Fomu hiyo ijazwe kikamilifu na Mganga katika Hospitali ya Serikali na muhuri ugongwe mahala panapohusika. Fomu iliyojazwa iwasilishwe na mwanafunzi siku ya kuripoti.

iii. Fomu ya kukubali kujiunga na shule. Fomu hii ina sehemu ya mzazi na sehemu ya mwanafunzi. Sehemu hizi zote zijazwe kikamilifu na fomu iwasilishwe na mwanafunzi siku ya kuripoti.

Karibu sana shule ya Sekondari Seuta.

.....

PETRO M. MWIKWABE
MKUU WA SHULE

HEADMASTER
SEUTA SECONDARY SCHOOL

KILINDI DISTRICT COUNCIL
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

THE HEADMASTER,
SEUTA SECONDARY SCHOOL,
P.O. BOX 30
SONGE – KILINDI

PART A
TO MEDICAL OFFICER
.....
.....
.....
.....

.....(**name in full**)
Please examine the above mentioned person as to his/her Physical and Mental fitness for a full time student. The examination should be as indicated below in PART B.

Date: ..... Signature.....

PART B:
MEDICAL CERTIFICATE
(To be complete by Government Medical Office)

I have examined the above named student and concluded that he/she is physically fit/until and mentally fit/until as a full time student.

I. (a). Eyesight.....
(b). Hearing.....
(c) Speech.....
(d) Limbs.....
(e) Venereal Diseases.....
(f) Leprosy.....
(g) Pregnancy.....

II. Neuroses.....
III. Other serious Diseases.....

Station:.....Signature.....

Date.....Designation.....

Stamp.....

HEADMASTER
SEUTA SECONDARY SCHOOL

HAMASHAURI YA WILAYA YA KILINDI
SHULE YA SEKONDARI SEUTA

YAH: KUKUBALI MASHARTI YA SHULE

SEHEMU A. SHERIA ZA SHULE (Zisomwe na mwanafunzi pamoja na mzazi)
Mambo yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa shule mara moja.

i. Wizi.
ii. Uasherati na ushoga.
iii. Ubakaji.
iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, mirungi, kubali, kokein, sigara pombe n.k.
v. Kupigana au kupiga.
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
vii. Kudharau bendera ya Taifa.
viii. Kuoa au kuolewa.
ix. Kupata mimba, kutoa mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule.
x. Kugoma, kuchochea, kuongoza, kushawishi au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
xi. Kuwa na simu ya mkononi.

SEHEMU B: (IJAZWE NA MWANAFUNZI
Mimi..... niliyechaguliwa kuanza masomo ya kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Seuta.

i. Ninakubali nafasi hiyo.
ii. Ninaahidi nitafuata sheria zote za shule zilizopo na kutakazokuja baadaye.
iii. Nitajiepusha na vitendo vyote ambavyo ni kinyume na taratibyu za shule.
iv. Nitakuwa mtiifu kwa walezi wangu wote shuleni ambao ni walimu na wafanyakazi wasio walimu.
v. Nitafuata maelekezo nitakayopewa na walimu na wafanyakazi wwengine wa shule na Viongozi wote watakaokuwepo kwa mujibu wa sheria.
vi. Ninaahidi kuwa kuwa nitatumia uwezo wangu na akili yangu kwa juhudi kubwa ili kupata mafanikio na matokeo mazuri katika masomo yangu.
vii. Nitahudhuria vipindi vya madomo darasani na nje ya darasa. Nitafanya mazoezi na mitihani yote nitakayopewa.
viii. Sitashiriki, kushawilshi wala kuongoza migomo au jambo lolote litakaloondoa/kuhatarisha amani ya watu.
ix. Nisipotekeleza yaliyotajwa hapo juu hatua zichukuliwe dhidi yangu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

Sahihi..... tarehe.....

SEHEMU C: (Ijazwe na Mzazi)
Mimi..... Ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi .....aliyechaguliwa kuanza kidato cha kwanza Seuta Sekondari mwaka 2021.

i. Nitasimamia mwanangu kuhudhuria shule kila siku ya masomo.
ii. Natambua kwamba utoro wa mwanangu shuleni utasababisha nichukuliwe hatua za kisheria hivyo nitawajibika kwa utoro wa mwanangu.
iii. Nitakagua madaftari ya mwanangu na kazi zingine za darasani (mazoezi na majaribio) ili nijiridhishe na ushiriki wa mwanangu na walimu katika kujifunza na kufundisha. Nitawasiliana na uongozi wa shule endapo kutakuwa na tatizo.
iv. Nitamhudumia mwanangu mahitaji yote ya shule ikiwa ni pamoja na madaftari, chakula, kalamu na sare za shule.

Sahihi yangu.....

Tarehe.....